

FORM 3 END TERM 2 2020

KISWAHILI PAPER 3

MAAGIZO:

- **Jibu maswali manne**
- **Swali 1 ni lazima**
- **Jibu maswali matatu kutoka kwa sehemu zilizobakia**

Kwa matumizi ya mtahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
SEHEMU YA A	20	
SEHEMU YA B	20	
SEHEMU YA C	20	
SEHEMU YA D	20	
JUMLA	80	

Kila mtahiniwa lazima aangalie kama kurusa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

SEHEMU YA A: USHAIRI

1. Soma shairi na kisha uyajibu maswali yafuatayo:-

1. Ni sumu, sumu hatari
Unahatarisha watoto
Kwa ndoto zako zako leweshi
Za kupanda ngazi
Ndoto motomoto ambazo
Zimejenga ukuta
Baina ya watoto
Na maneno laini
Ya ulimi wa wazazi

2. Ni sumu, sumu hasiri
Unahasiri watoto
Kwa pupa yako hangaishi
Ya kuwa tajiri mtajika
Pupa pumbazi ambayo
Imezaa jangwa bahili
Badala ya chemicchemi
Ya mazungumzo na maadili
Baina ya watoto na mzazi

3. Ni sumu, sumu legezi
Unalegeza watoto
Kwa mazoea yako tenganishi
Ya daima kunywa ‘moja baridi’
Mazoea mabaya ambayo yanafunga katika klubu
Hadi saa nane usiku
Huku yakijenga kutofahamiana
Baina ya watoto na mzazi

4. Ni sumu, sumu jeruhi
Unajeruhi watoto kwa pesa,
Kwa mapenzi yako hatari
Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi
Na kisha kwenye madawa ya giza baridi
Barabara inayofikisha kwenye giza baridi la kaburi la asubuhi

Maswali

- (a) Pendekeza kichwa kwa shairi hili. (**alama 1**)
- (b) Fafanua maudhui ya shairi hili. (**alama 2**)

- (c) Ni kwa njia gani kinachozungumziwa kinajenga ukuta? . **(alama 2)**
- (d) Dondoa tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi na uztoloo mfano **(alama 4)**
- (e) Eleza umbo la shairi hili. **(alama 3)**
- (f) Uandike ubeti wa nne kwa lugha nathari. **(alama 4)**
- (g) Eleza maana ya vifungu hivi viliviyotumika katika shairi . **(alama 4)**
- (i) Giza baridi
- (ii) Yanakufunga katika klubu

SEHEMU YA B: KIDAGAA KIMEMWOZEA

2. Jadili umuhimu wa mbinu ya majazi kwa kurejelea jina Sokomoko. **(alama 20)**
3. “alisimama jadidi na kuwatazama hawa watu wawili waliosimama wima kutetemeka kama waliokuwa wamepigwa na dhoruba ya theluji.”
- a) fafanua muktadha wa dondo hili **(alama 4)**
- b) taja mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondo hii.**(alama 4)**
- c) onyesha umuhimu wa ‘anayesimama jadidi’ katika kuijenga riwaya hii.**(alama 12)**

SEHEMU YA C:MSTAHIKI MEYA

- 4.“..wewe hukubaliani na chochote siku zote. Kauli yako ndiyo waiona kuwa yenyе hoja inayoistahili kufuatwa.”
- a) Fafanua muktadha wa dondo hili. **(alama 4)**
- b) Eleza nyakati zingine ambapo wahusika hawa wawili walitofautiana.**(alama 16)**

5.Taja na ueleze njia anazozitumia Meya katika kuuendeleza uongozi wake. **(alama 20)**

SEHEMU YA D:DAMU NYEUSI NA HADITHI ZINGINE

6. “ si udufu kitu gani,mtu aache kutukia nyayo za kweli.....”
- a) Eleza muktadha wa dondo hili **(alama 4)**
- b) Jadili hulka na umuhimu wa msemaji **(alama 16)**

7.Kwa kulejelea hadithi tofauti katika diwani ya Damu nyeusi na hadithi nyingine, jadili maudhui haya: **(alama 20)**

- a) Ubaguzi
- b) Ndoa
- c) Umaskini

SEHEMU E:FASIHI SIMULIZI

8. a) Taja na ueleze sifa za mtambaji bora katika fasihi simulizi. **(alama 10)**
- b) Nyimbo zina wajibu gani katika jamii. **(alama 4)**
- c) i) Eleza maana ya vitendawili. **(alama 2)**

ii) Onyesha sifa za kitendawili. (**alama 4**)

9. a) Taja na ueleze aina nne kuu za hadithi (**alama 8**)

b) Eleza mbinu tatu ambazo mtambaji anaweza kutumia kuishirikisha hadhira yake. (**alama 6**)

c) Fafanua viperu vifuatavyo vya fasihi simulizi. (**alama 6**)

i) Majigambo

ii) Mivigha

iii) Lakabu